Kasarani Campus
Off Thika Road
P. O. Box 49274, 00101
NAIROBI
Westlands Campus
Pamstech House
Woodvale Grove
Tel. 4442212
Fax: 4444175

# KIRIRI WOMENS' UNIVERSITY OF SCIENCE AND TECHNOLOGY

UNIVERSITY EXAMINATIONS, 2022/2023 ACADEMIC YEAR
END OF SEMESTER EXAMINATIONS
FOR THE DEGREE OF BACHELOR OF EDUCATION (ARTS)

## KSW 2403;POETRY

Date: 13th December, 2022
Time:2.30pm-4.30pm

**MAAGIZO:JIBU SWALI LA KWANZA NA MENGINE MAWILI**

**SWALILA KWANZA. (ALAMA 30)**

a)Taja na ueleze tofauti kati ya ushairi na tanzu zingine z afasihi. (Alama 6)

b)Eleza muundo wa nje wa ushairi. (Alama 4)

c) Fafanua aina ya mashairi katika lugha ya Kiswahili. (Alama 6)

d)Ainisha dhana ya muundo katika ushairi. (Alama 6)

e)Eleza matumizi ya lugha katika Ushairi. (Alama 4)

f) Fafanua umuhimu wa fasihi katika jamii (Alama 4)

**SWALI LA PILI. (Alama 20)**

a)Jadili maudhui yanayojitokeza katika utendi wa mwana kupona. (Alama 10)

b)Fafanua misimamo ya wanajadi kuhusu ushairi. (Alama 10)

**SWALI LA TATU. (Alama 20)**

a)Tathmini mambo makuu yanayojitokeza katika mashairi ya Shaban Robert. (Alama 8)

b) Jadili fani katikaUshairi. (Alama 8)

c)Jadili msimamo wa wanausasa kuhusu ushairi (Alama 4)

**SWALI LA NNE. (ALAMA 20)**

A)Tathmini misimamo ya wanausasa kuhusu ushairi wa Kiswahili. (Alama 10)

b)Eleza maudhui yanayojitokeza katika ushairi wa Kinge'I kama mwanausasa. (Alama 6)

c) Eleza muundo wa ndani waushairi (Alama 4)

**SWALI LA TANO. (ALAMA 20)**

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo.

1. Naja sasa ni ndayani, naja kwetu Mzalendo
Naja ninarudi nyumbani, nilowekwa na kokando
Kwetu mi nakutamani ,kulo na mwingi uhondo
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini

2. Naja kwingine kuwapa, kulojaa langu pendo
Huenda nenda kwinginepo,sawa nako wa muundo
Kaa kwingine anapi, ela kwenye lakwe gando
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharani.

3 .Naja nije rudi papo, panigendeme mgando.
Ningaambwa kwetu hapo, kwamba kwanuka uvundo
Sitakwenda penginepo, tarudi kuko kwa mwando
Nijaye ni ile nyundo,misumari hadharani.

4.Naja sitapakimbiya, ningambwa kuna vimondo.
Takuja kuvilekeya, vinganijia kwa vundo
Nilipozawa tafiya, sikimbii kwenda kando
Nijaye ni ile nyundo, msumari hadharani.

5.Naja hiwa mekomaa, kuzidi nilivyo mwando.
Tena n’najiandaa, kwa fikira na vitendo
Kwetu nije kuifaa, na kuitiliya pondo
Nijaye ni ile nyundo, msumari hadharini.

6.Naja naingawa naja ,siwaekei mifundo
Moyo wangu ushatuja, mawi nalotendewa mwando
Ela wataoningoja,na vyao viwi vitendo
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini

a) Eleza muundo wa shairi hili. (Alama 4)

b)Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu zako (Alama 6)

c)Jadili uhuru wa kishairi uliotumika katika shairi hili. (Alama 6)

d)Fafanua maudhui matatu yanayojitokeza katika shairi hili (Alama 4)